Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 5, Issue 3

11th Muharram 1432

17th December, 2010

Yaliyomo

Hali Ya Umma Wa Ki-Islamu Ilivyo 1 - 3

Damu Asilia Za Kina Mama 3 - 4

HALI YA UMMA WA KI-ISLAMU ILIVYO

Mtayarishi: Sheikh Salim Bin ‘Eid al-Hilaali

Imedhihirika katika zama zetu hizi yakwamba Umma wetu wa ki-Islamu unasononeka na kudhalilika kutokamana na maafa. Na ni maafa hayo ambayo yaliyousababisha umma huu kudhoofika na kushindwa kusimama juu ya uadilifu. Maafa yenyewe ni kama yafuatayo:

HALI YA UDHAIFU:

Tumekwisha kuelezwa kuhusu hali hizi, na tukatahadharishwa waziwazi pasi na kufichwa pakawa hamna udhuru wa kuwa ati sisi hatukujua (ujinga). Thawbaan (رضي الله عنه), mmoja miongoni mwa wafanyi kazi (watumishi) wa Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) akasema yakwamba amesema Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) *"Hivi karibuni mataifa yataitana kuungana dhidi yenu, kama vile watu wanavyoitana kuja kula kutoka kwenye sinia ya chakula."*

Akauliza mtu mmoja: "Litakuwa jambo hilo kwa ajili ya idadi yetu itakavyokuwa chache, Yaa Mtume (صلى الله عليه وسلم)?"

Akajibu Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Laa, mutakuwa idadi yenu ni kubwa, lakini mutakuwa ghuthaa'a kama zile takataka za povu zinazo-olea juu ya kidimbwi cha maji, na Allaah (سبحانه وتعالى) ataondoa khofu kutoka katika nyoyo za maadui zenu (ya kuwaogopa nyinyi) na atawaekea kwenye nyoyo zenu WAHN."*

Wale waliokuwepo pale wakauliza: "Na ni nini hiyo WAHN, ewe Mtume (صلى الله عليه وسلم)?"

Akajibu Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Ni kuyapenda maisha ya kidunia na kuyachukia mauti."* [Hadeeth Saheeh kwa kutokamana na njia nyingi za upokezi katika Sunan ya Aboo Daawood (4297)]

Hadeeth hii ifuatayo inatufahamisha vizuri sana hiyo hali ya WAHN:

KWANZA: Maadui zetu, ambao ni wenyeji wa Iblees na watumishi wake, wamejaribu sana kuyapinga maendeleo ya Ummah na kunyakuwa kutoka katika ardhi zake wanapo-ona yakwamba wahn imetuingilia na kutusibu. Tangu kupambazuka kwa Uislamu mpaka hivi leo, tunawaona makuffaar na mushrikeen kutoka kwa walio miongoni mwa watu wa kitabu wakijitahidi mno vitimbi vyao dhidi ya Waislamu. Wamejaribu daima dawama kutafuta njia za kuonyesha yakwamba watu wetu ni wanyonge. Walijaribu kufanya vitimbi hivyo hata katika mji ulioimarishwa na kulelewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Imeelezwa wazi habari hii katika kisa cha "Watu watatu waliosusiwa" (Tizama Surat at-Tawbah :118). Akasema Ka'b bin Maalik (رضي الله عنه): *"...Na nilipokuwa nikitembea kwenye sehemu za soko la Madeenah, nilimkuta mkulima mmoja aliyekuwa ni miongoni mwa waliokuja na msafara wa kibiashara uliokuja kutoka Shaam, aliekuwa akiuza baadhi ya vyakula alivyovileta. Mtu huyo alikuwa akiniulizia wapi atanipata mpaka akaelekezwa kwangu. Kisha akanipa mimi barua yangu iliyotoka kwa mfalme wa Ghassaan. Kwa vile mimi nilikuwa ni msomi, niliisoma, nayo ilisema: "Kwanza kabisa; Zimetufikia habari sisi yakwamba rafikiyo (Muhammad (صلى الله عليه وسلم) amekutupilia mbali na hana haja na wewe. Allaah hakutakii wewe kubakia kwenye nchi ya kudhalilishwa. Njoo kwetu nasi tutakuhifadhi."* [Imeafikiwa]

Ewe Muislamu, hebu tafakari na kuzingatia juu ya vile walivyo makuffaar, wale waliozivirinqa nchi za ki-Isalmu, wanavyopokea habari za mambo yanayotokea ndani ya miji yetu. Wamekaa wakisubiri, huku wakiwa wamejiandaa kutaka kutushambulia kwa ghafula. Mifano ifuatayo yaonyesha wazi njama hizo zao.

PILI: Mataifa ya kikafiri wanaitana wenyewe kwa wenyewe na kuunda majeshi ya ushirikiano wakiwa na lengo la kuuangamiza Uislamu na mwito wake, watetezi wake na miji yao. Mambo hayo yanaonekana waziwazi katika Crusade (vita vya Wakristo juu ya Maturuki) na vita vya kwanza vya Ulimwengu (First World War). Katika vita vya kwanza vya Ulimwengu, lengo lao kubwa lilikuwa ni kuondolea mbali Khilaafah. Katika kuyashughulikia malengo yao ya ufisadi, mataifa ya makafiri walijiandaa wenyewe kwanza kama chama, kisha kikageuka chama na kuwa kundi moja kubwa zaidi, na likazidi kustawi mpaka hatimae wakaweza kuiimarisha Amri Mpya ya Ulimwengu - (New World Order).

TATU: Kwa hakika, ardhi nyingi za Waislamu ni machimbuko ya madini ya thamani ya Ulimwengu. Kwahivyo, mataifa hayo ya makafiri wanakusudia kutunyang'anya ardhi zetu ili wawe na uwezo juu ya madini hayo. Hivyo basi, tunaona jinsi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivyowasifu kama kwamba wanaitana wao kwa wao katika karamu. Kila mmoja wao akipigania sehemu kubwa ya kinyang'anyiro.

NNE: Mataifa ya makafiri wanagawanyiana katika baraka za miji yetu, bila ya kuogopa lawama wala kulipa kisasi. Isitoshe, kisha mali hizo huchukuliwa, ema kwa nguvu au kwa khiyari.

TANO: Mataifa ya makafiri watazikuta

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

ardhi zetu na majeshi yaliyotawanyika kila sehemu. Mas-ala haya yamefafanuliwa katika hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) iliyopokewa na 'Abdullaah bin Hawaalah (رضي الله عنه)aliesema yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Mutakuwa kikundi cha Askari na Jeshi. Kikundi cha Jeshi kitakuwepo Shaam, kikundi chengine kitakuwepo Iraaq, kikundi chengine kitakuwepo Yemen."*
Nikauliza: "Hebu nichagulie, ewe Mtume (صلى الله عليه وسلم) nijiunge na kikundi kipi?"
Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Nenda Shaam... kwa hakika, Allaah (عز وجلَ) Ameudhamini usalama wa mji wa Shaam na watu wake."*
Rabee'ah, ambae ni miongoni mwa wapokezi wa hadeeth hii, ameeleza yakwamba amemsikia Aboo Idrees Al-Khiwalaani akiisimulia hadeeth hii kisha akasema: "Alichokiapia Allaah kukilinda, hapana awezae kukiangamiza." [Saheeh]
Hii inaonyesha waziwazi hali vile ilivyo ya Ulimwengu wa ki-Islamu. Ndani yake zikipatikana nchi tafrani zisizoweza kujiimarisha kwa chochote: ikiwa ni hali yao ya ndani au hata mas-ala ya nje ya nchi. Wanajipatia uhuru wao, ulinzi na kujiimarisha kutoka kwa mataifa ya makafiri.

SITA: Mataifa ya ma-Kuffaar hawajishughulishi kamwe na, licha ya kuwaogopa, Waislamu. Ile khofu waliyowahi kuwa nayo wakati fulani katika nyoyo zao hawana tena. Uwoga ambao siku zilizopita uliosababisha nyoyo za mataifa ya makafiri kutetema na kuogopa hauna maana yoyote - kama ungalipo angalau chembe.
Allaah (سبحانه وتعالى) Amesema kama ilivyofasiriwa: "**Tutatia khofu katika nyoyo za wale waliokufuru, kwa sababu ya kumshirikisha kwao Allaah na (wale waungu wao wa batili) ambao Hakuteremsha dalili (ya uungu wao).** [Soorah Aali Imraan 3:151]
Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) akasema: *"Nimepawa ushindi kutokana na khofu walizonazo maadui zetu juu yetu, (ambao) uliotutangulia umbali wa safari ya mwezi mzima."* [Imepokewa na al-Bukhaaree (Vol.1 uk.436 Fat-h) na Muslim (# 521 kutoka katika hadeeth ya Jaabir bin 'Abdullaah].
Hii ni sifa hususan iliyopewa kwa Ummah wetu. Na imethibitishwa katika hadeeth ya Thawbaan (رضي الله عنه): *"Na Allaah (سبحانه وتعالى) ataondoa khofu kutoka katika nyoyo za maadui zenu (ya kuwaogopa nyinyi)."*

SABA: Mas-ala mengine yenye umuhimu ni kwamba, Ummah hauongezeki nguvu kwa idadi kubwa wala kwa silaha walizonazo. Nguvu za Ummah ziko kwenye 'aqeedah yake na kwa wale walioshikamana na Tawheed. Kwani hatukumsikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: **"Kwa hakika, idadi yenu mutakuwa wengi"**. Na hatujata'amali mafunzo yafuatayo ambayo yatakayobaki milele katika zama zote, Aliposema Allaah (سبحانه وتعالى) kama ilivyofasiriwa: "**Na siku ya Huneyni (pia); ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni chochote.** [Soorat at-Tawbah 9:25]

NANE: Hamukujali wala kuwa na mazingatio juu ya Ummah wenu, kama vile alivyobashiri Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema: *"Mutakuwa ghuthaa'a kama zile takataka za povu zinazo-olea juu ya kidimbwi cha maji."*Ushahidi wa alama tulizokwisha kuzitaja zinatufahamisha yafuatayo:

1. Kidimbwi cha maji ndicho chenye kuizuiya ghuthaa'a inayo-olea. Na hivyo ndivyo Ummah wetu ulivyo siku hizi. (Ummah wetu) uko katika msururu mmoja na mataifa ya makuffaar, ambao wamewatawala kikamilifu na kuwaweka chini ya himaya yao.

2. Katika ghuthaa'a kuna vitu visivyokuwa na thamani yoyote kwa wana-adamu. Na hiyo ndiyo hali ya Ummah wetu leo. Ummah umetupilia mbali vitendo ambavyo vilivyo-uhifadhi ufanisi wake, haswa kuamrisha mema na kukataza maovu.

3. Ghuthaa'a hupita njia pasi na kuacha athari zozote. Allaah (سبحانه وتعالى) daima huleta kheri kutoka kwenye shari na akaleta watu wema watakaokuwa ndio asili ya uongofu na kheri nyingi kwa mwana-adamu.

4. Kila mara, ghuthaa'a itabeba uchafu. Na hayo ndiyo mafundisho ya upotofu yaliyotambaa na kuingia ndani ya fahamu za Waislamu wengi kutokamana na mafunzo ya dini nyengine.

Kwavile ghuthaa'a haina budi kuwa chini ya nguvu za mfumo, basi inakuwa haijijui itamalizikia wapi. Huwenda ikawa Ummah hautambui kuhusu mipango au njama zilizopangwa na maadui zao, na isitosha, wakawa wanauitika mwito wa kila mlinganizi, bila ya kupima thamani za miito yenyewe.

TISA: Leo, Ummah huu, katika zama zetu umeyafanya maisha ya kidunia kuwa ndiyo malengo yetu na mambo yenye kufaa kushughulikiwa kuliko kitu chochote. Na ni kwa ajili hii ndio wakawa wanayaogopa mauti na matokeo yake. Wanayapenda mno haya maisha waliyoyazamia ya kidunia; wamejisahaulisha kabisa umuhimu wa maandalizi ya Aakhera. Jambo hili ni miongoni mwa mambo ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyoyahofia kwa Ummah huu. Akapokea 'Abdullaah Ibn 'Amr bin al-'Aas (رضي الله عنه)kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa alisema: *"Mutakapowapiga wa-Fursi na wa-Rumi, mutakuwa ni watu wa aina gani?"*
Akajibu 'Abdur-Rahmaan bin 'Auf (رضي الله عنه): "Tutasema kama alivyotuamrisha Allaah."
Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu: *"Au jambo jengine lisilokuwa hilo. Mutaanza kushindana wenyewe kwa wenyewe, kisha muoneane wivu wenyewe kwa wenyewe, kisha mufanyiane vitimbi wenyewe kwa wenyewe, kisha muchukiane wenyewe kwa wenyewe. Baada ya hayo, mutawaendea muhaajireen mafukara na muwasababishe waanze kupingana."* [Saheeh Muslim : 2962].

Ndio kwa ajili hii tumeona wakati wa-Fursi walipopigwa, 'Umar ibn al-Khattaab (رضي الله عنه) akaanza kulia na akasema: "Hapana watakaopewa haya isipokuwa wale watakaoanza kugombana wenyewe kwa wenyewe."

KUMI: Ni lazima itangazwe yakwamba mataifa ya makafiri hawatoweza kuuangamiza Ummah. Hata kama watashirikiana kwa umoja wao wanapoazimia kufanya hivyo. Katika

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

hadeeth nyengine iliyopokewa na Thawbaan (رضي الله عنه), tunaona yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Allaah (سبحانه وتعالى) aliibana ardhi yote ili mimi nipate kuiona mashariki na magharibi yake. Kwa hakika Ummah wangu utaenea kote ulimwenguni. Nimepewa hazina mbili, nyekundu na nyeupe (dhahabu na fedha, hazina za wa-Fursi na wa-Rumi). Nikamuomba Mola wangu Asiuangamize Ummah wangu kwa ukame. Vilevile nikamuomba Asiwaletee adui dhidi yao mbali na asiekuwa wao wenyewe, wala yeyote atakaewaondolea umoja wao na nguvu zao."* Akasema Mola wangu: **"Ewe Muhammad! Ninapokadiria amri yoyote basi haiwezi kukataliwa. Nimekukubalia maombi yako kwa niaba ya Ummah wako, yakwamba wasifikwe na mkasa wa ukame. Sitowaletea adui asiyekuwa miongoni mwao atakaewaondolea umoja wao na nguvu zao, hata kama mataifa yote yataungana dhidi yao. Hali hii itabakia hivyo mpaka watakapoanza kuangamizana wao kwa wao na kuapizana wenyewe kwa wenyewe."** [Saheeh Muslim : 2962]

NENO LA BUSARA

Katika swaheeh yake (2581), Muslim akapokea kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliuliza: *"Munamjua nyinyi ni nani [mtu] muflis?"* Wakasema, "kulingana na ujuzi wetu, [mtu] muflis ni yule ambaye asiyekuwa na dirham [pesa] wala kitu chochote." Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaambia: *"Hakika mtu muflis katika Umma wangu atakuja siku ya Qiyaama akiwa ameswali, amefunga na ametowa zakaah, na atakuja haliyakuwa amemshutumu huyu, akamsingizia huyu, akala mali ya huyu, akamwaga damu ya huyu, na akampiga huyu. [Kwahiyo mtu huyu] atalipwa kutoka katika mema yake na huyu atalipwa kutoka katika mema yake. Kisha ikiwa mema yake yamemalizika kabla hajamaliziwa hisabu yake [akawa bado amedhulumu watu] yatachukuliwa makosa ya wale [alowadhulumu] abandikiziwe nayo yeye, na kisha atumbukizwe motoni."*

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 4)

4. Jee kama mturuziko wa damu ya Nifaas umesimama kabla ya muda wa siku arubaini na kasha ikarudi tena katika siku ya arubaini? Kinyume cha damu ya heidh1, hali hii ya kurudi tena inazingatiwa kuwa na "Shaka" kulingana na misemo mashuhuri ya Wanavyuoni wa ki-Hanaabila. Yeye (huyu mwanamke), kulingana na mtizamo wao ni lazima aswali na afunge kwa wakati wake. Kila alichoharamishiwa mwenye heidh, vilevile kimeharamishwa kwake, isipokuwa vitendo vilivyo waajib. Itamlazimu alipe yote yale yatakayomlazimu mwenye heidh kulipa. Hatahivyo, muandishi huyu yuko juu ya rai yakwamba: "Iwapo damu itamrudia akiwa ndani ya muda ambao hwenda ukawa ni muda wa Nifaas, basi damu yake ni damu ya Nifaas. Lau si hivyo, basi itakuwa ni damu ya heidh, isipokuwa iwapo itaendelea kumtoka ndio hapo itakapokuwa ni damu ya Istihaadhah. Rai hii imekurubiana na ile iliyonukuliwa katika Al-Mughnee (V. 1, Uk. 349) ambapo imetajwa yakwamba Imaam Maalik alisema: "Ikiwa ataiona damu siku mbili au tatu baada ya kusimama kutoka kwake, basi hiyo itakuwa ni damu ya Nifaas, au kinyume chake itaqkuwa ni damu ya heidh." Hili pia ndilo chaguo la Ibn Taymiyyah.

Kwa uhakika, hakuwezi kuwa na "shaka" kuhusu damu. Hatahivyo, ni suala lenye kuhusiana ambamo rai za watu huwenda zikatafautiana kulingana na ilimu zao na ufahamu wao. Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم) ndizo asili za ubainifu wa kila jambo. Allaah (سبحانه وتعالى) hakuwajibisha kwa mtu afunge mara mbili na kufanya Twawaaf mara mbili isipokuwa ikiwa kuna jambo lililofanywa kwa makosa wakati wa utekelezaji wa vitendo hivyo kwa mara ya kwanza na kwamba haiwezi kurekebishika bila ya kulipa. Hatahivyo, Ikiwa damu ya heidh imesimama kisha ikarudi tena, basi hapana shaka yakwamba hiyo ni damu ya heidh. Kwa mfano, mwanamke amepata damu yake ya kawaida ya kila mwezi kwa siku nane. Anasema yakwamba damu inasimama katika siku ya nne kwa siku mbili, kisha ikarudi tena kutoka katika siku ya saba na nane. Damu hii iliyorudi tena hapana shaka yakwamba ni damu ya heidh. katika hali ya mtu anapofanya kitendo fulani kadiri ya uwezo wake (mke au mume), basi huwa mtu yule hakalifishwi kutokana na majukumu yoyote kama alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى): "**Allaah hamkalifishi mtu yoyote isipokuwa lile..."** (Al-Baqarah 2:286)

"Mcheni Allaah kadiri ya uwezo wenu." (at-Taghaabun 64:16).

5. Jee kuingiliana na mwanamke aliyetwahirika kabla ya siku arubaini za marejeo-ya-muda wa Nifaas? Katika hali ya mwenye heidh, inaruhusiwa kuingiliana nae iwapo atasafishika kabla ya muda wake "wa kawaida" wa ada yake. Katika hali ya Nifaas na kulingana na rai maarufu ya madh-hab ya Hanbalee, kuingiliana ni makuruhu. Hatahivyo, rai ya sawa ni kwamba si makuruhu na huu ndiwo msimamo wa wanavyuoni wengi wa ki-Islamu, kwa sababu kufanya jambo kuwa ni makuruhu kunahitaji ushahidi utakaosaidia kutoka katika sheriya ya Uislamu. Katika hali hii, hakuna ushahidi isipokuwa yale yaliyopokewa kutoka kwa Imaam Ahmad: "Mkewe 'Uthmaan, mtoto wa Abee Al-'Aass alimjia kabla ya kumalizika kwa muda wa siku arubaini na akamwambia: 'Niwache!'". Hii hailazimu kwamba alichukizwa aliyoyafanya kwa sababu yawezekana yakwamba alikuwa akijichunga akihofia kutokuwa na hakika kwamba alikuwa ashatwahirika (kutokamana na Nifaas) au kwamba huwenda kutokwa na damu kukaanzishwa upya baada ya kuingiliana nae au kwa sababu nyengine na Allaah Ndiye Mjuzi Zaidi.

KUTUMIA VIZUIZI VYA HEIDH NA MADAWA YA KUAMSHA HISIYA:

Matumizi ya vyenye kuzuiya heidh yanaruhusiwa chini ya masharti mawili:

La Kwanza: Yasipatikane madhara kwa mwanamke. Kwa sababu amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na wala musijiangamize nafsi zenu"** (al-Baqarah 2:195).

"Wala musijiuwe nafsi zenu. Hakika Allaah daima kwenu ni Mwenye Huruma." (an-Nisaa' 4:29)

La Pili: Ikiwa matumizi yake yatamuathiri mume kwa njia moja au...

[Endelea Katika Makala Yajayo]

[Endelea Kutoka Vol 3, Issue 4]

Muandishi huyu amesema: "Kutokana na hayo yaliyo hapo juu, ikiwa damu itaendelea kumtoka mwanamke zaidi ya masiku arubaini na ikiwa kutapatikana alama zenye kuashiriya yakwamba damu hiyo itasimama kutoka (kutokamana na mimba zilizotangulia na alama nyengine), basi itambidi asubiri mpaka mturuziko wa damu usimame. Iwapo mwanamke hakupata dalili hizo, basi atajisafisha (kwa kuoga), baada ya kukamilika siku arubaini akiuzingatia muda huo kuwa ni wa marejeo kwa wanawake wengi. Kwa upande mwengine, iwapo akimaliza masiku arubaini, mara akapata ada yake ya kawaida ya kila mwezi, hapo atasubiri mpaka imalizike. Iwapo damu itaendelea baada ya ada yake ya kawaida kumalizika, basi yeye atakuwa ni 'Mustahaadhah' na atafuata hukmu za Istihaadhah.'"

Ikiwa damu ya Nifaas itasimama kabla ya marejeo-ya-muda ya siku arubaini na akasafishika, basi ataoga, aswali, afunge na anaweza kujamiiyana na mumewe. Kusimama kwa mturuziko wa damu kwa uchache wa siku moja hakumruhusu (mwanamke) kusafishika.

Nifaas haithibitishwi mpaka mwanamke azae kiumbe aliyekamilika. Ikiwa mwili mdogo umezaliwa lakini ukawa hauonyeshi umbile linaloendelea kukuwa la mwana-adamu, basi damu husika inayotoka hapo si Nifaas na huzingatiwa kuwa ni damu ya 'Irq (damu itokayo kwenye mshipa). Muda mchache kwa umbile la mwana-adamu kuweza kukuwa ni siku thamanini kuanzia siku ya kutungika mimba na kwa mara nyingi ni siku tisiini.

Ibn Taymiyyah amesema: "Ikiwa ataona damu inayoungana na kubanwa kwa misuli kabla ya siku thamanini au tisiini, asijali chochote (yaani; na aendelee kuswali na kufunga), lakini lau ataona damu baada ya muda huu, basi atajiepusha na kuswali na kufunga. Hatahivyo, iwapo, ataubwaga mzigo wake (atazaa), na mzaliwa mpya akawa ana umbile linaloendelea kukuwa la mwana-adamu, basi damu yake itokayo (kabla ya siku thamanini au tisiini) na izingatiwe kuwa ni Nifaas na asawazishe siku zake kwa kuswali na kufunga. Ikiwa kwa upande mwengine mzaliwa mpya haonyeshi umbile linaloendelea kukuwa la mwana-adamu, basi damu yake itokayo iendelee kutozingatiwa kuwa ni Nifaas, na wala hatokuwa na haja ya kulipa swala zake na Saumu."

SHERIYA ZA NIFAAS:

Sheriya za Nifaas ni sawa na sheriya zinazohukumu heidh, isipokuwa katikamas'ala yafuatayo:

1.Eda haihusiani na Nifaas, lakini, kwa usahihi zaidi, inahusiana na hukmu za Talaka. Kwa mfano: ikiwa talaka ilitolewa kabla ya mazazi, basi Eda itakwisha baada ya kuzaa na wala haihusiani na muda wa Nifaas. Iwapo Eda ilitolewa baada ya mazazi, (mzazi) atasubiri irudi heidh yake na kama ilivyo ahesabu Eda yake kama ilivyoelezwa hapo awali.

2. Muda wa Eelaa': Eelaa' ni, Mume akiapa kutomuingilia mkewe milele (au kwa zaidi yab miezi minne). Lau mkewe atahitaji kujamiiana nae, muda wa miezi minne kuanzia siku aliyoapa kiapo chake, utadhibitiwa. Muda huu ukamilikapo, ataamrishwa (na hakimu ya Ki-Islamu), ema atekeleze kitendo cha kumuingilia mkewe au maombi ya kutenganishwa yatatekelezwa na mkewe. Nifaas haitohesabiwa kuwa dhidi ya muda wa Eelaa'. Nyongeza ya muda ulio sawa na muda unaohitajika kwa twahara ya mke kutokamana na Nifaas utaongezwa kwenye muda wa Eelaa'. Hii ni kinyume cha heidh, ambapo muda wake unahesabiwa dhidi ya muda wa Eelaa'.

3. Kubaleghe: Ni dhahiri yakwamba Nifaas inahusiana na mimba. Mwanamke hawezi kupata mimba kabla ya kupata aina fulani ya shahawa za kijinsia (sexual secretions) kutoka mwilini mwake. Heidh (na wala si Nifaas) ni ishara yakwamba umetimia umri wa kubaleghe.

KILIFI BOOKS & STATIONERY STORE LTD

Executive Director: Muhammad A. Said

Suppliers of: *School Textbooks & Stationeries, Office Stationeries, Films, Dealers of AirTel Cards and Safaricom Cards.*

* Madrasatul Munawwar Wakf Building—Mombasa
* Jamo Kenyatta Avenue—Mombasa
* Hospital Street—Opposite P.H.D Mombasa.

P.O.Box 99900 *Tel: 041-2495763*

Postal Code: 80107 *Fax: 041-2495764*

E-mail:kilifibks@africaonline.co.ke *Mobile: 0722-265103 / 0722-669414*